Shule ni elimu?

Jishindie kompyuta ndani!

Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza

Waandishi:
Richard Mabala na Winston Churchill Shauri

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Rakesh Rajani, Evarist Kamwaga, Joseph Ngwegwe na Justice Rutenge

Usanifu:
Winston Churchill Shauri

©Tamasha/Twaweza 2012

Barua: S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania
Simu: +255 719 751 928
+255 787 220 233

Barua pepe: rmabala@yahoo.com
wchachi@yahoo.com

Tovuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Tangu Uhuru, serikali imejitahidi kuongeza idadi ya shule nchini ili kuwawezesha watoto wote kusoma. Mwanzoni ilijikita zaidi katika elimu ya msingi, lakini kuanzia 2006, imeweka msisitizo kwamba kila kata iwe na shule yake ya sekondari. Hivyo, kwa mujibu wa MKUKUTA (2010):

- Shule za sekondari za serikali 2,171 zimejengwa kati ya 2005 na 2010
- Idadi ya wanafunzi wanaosoma sekondari imeongezeka kutoka 524,325 (2005) hadi 1,638,669 (2010)
- Zaidi ya nusu ya watoto waliomaliza shule ya msingi walipata nafasi katika shule za sekondari.

Hayo ni mafanikio makubwa. Lakini sasa tuhakikishe kwamba shule hizo zote zinawawezesha watoto na vijana kufikia ndoto zao za maisha, badala ya kuwakatisha tamaa kutokana na ufinyu wa elimu inayotolewa. Ingawa utafiti umethibitisha kwamba mafanikio za shule hayatokani tu na uwepo wa walimu na zana, ni dhahiri kwamba kukosekana kwao kunaathiri sana uwezekano wa kupata elimu. Na hadi sasa kuna uhaba mkubwa sana wa walimu, vitabu na zana zingine, na majengo muhimu kama vile maabara. Aidha, utafiti umeonyesha wazi kwamba wanafunzi walio wengi sana hawana Kiingereza cha kutosha kuweza kusoma masomo yote kwa lugha hiyo.

Ingawa si kipimo pekee, matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne yanadhihirisha kwamba shule haziwawezeshi watoto ipasavyo. Katika matokeo ya mwaka 2010, 88% ya wanafunzi walipata daraja la nne au sifuri[1].

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha

1 Baraza la Mitihani

Wahusika

Bonge: Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo

Bibiye: Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Mwenyekiti: Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mtendaji: Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Mwanakijiji: Mwalimu mkuu mstaafu mwenye azma ya kusaidia kuinua elimu kijijini

Duh! divisheni ziro.
Wote sifuri, sifuri sifuri, sifuri...!
matokeo.
Yaani nimepoteza miaka minne kwa ajili ya kulamba sifuri tu!?

Haiwezekani nakwambia. Shule si shule. Bora tuifunge
funga!
funga!
funga!

Nini tena jamani?
Hamjaona matokeo?
Acha tu! Unakumbuka nilikuwa naongoza darasani? Nikaishia kupata D mbili tu!

Sasa mnataka kufunga shule? Kwani shule ina kosa?
Bora kuonyesha hasira zetu. Haiwezekani shule nzima Sifuri tu!
Walimu hakuna. Vitabu hakuna. Shule ina faida gani?

Unajua wazazi wetu waliwekeza jasho lao kiasi gani? Hadi damu yao!
Miaka minne bure. Aaah! Tufanye nini?
Hilo ndilo swali...

Tunapinga sana hii elimu mbovu mzee wangu.
Mnashtuka leo? Mlikuwa hamjui shule yenu ni mbovu? Mlichukua hatua gani?

Kwani sisi wazazi? Hata tukisema hatusikilizwi!
Basi tusaidiane. Hata wazazi tumekereka.
Tushalalamika sana.


Njooni mniokoe!
Baba anataka
kunitoa shuleni.
Haiwezekani.
Twendeni
tukamsaidie.

Asante mwalimu. Ni kwa faida yake tu!
Kuna nini hapa? Hata shule mnawaozesha wanafunzi?
Mnataka nini? Tokeni!

Bora kuolewa kuliko kukaa bure miaka minne! Hii ni shule kweli?
!
Ina maana tumeshindwa shule kabisa? Elimu ni ufunguo lakini shule imeupinda.

Na hizi pesa ni za nini? Hatukubali!
Tuzipeleke kwa mtendaji. Watajibu huko!

OFISI

Baada ya siku tatu kuna mkutano wa kijiji
Wananchi, hali ya shule yetu si shwari. Mmeona matokeo ya mitihani. Mmesikia mwalimu mkuu amekamatwa. Hebu kwanza tuwasikilize vijana wetu wanasemaje.

Vijana wanaonyesha igizo


Igizo linaendelea
Who can explain me a cockroach?

Stupid. Stupid. Stupid you will all fail, isn't it?
Lakini siyo kosa letu mwalimu. Tumefundishwa Kiingereza saa ngapi?
Kwanini tusifundishwe kwa lugha tunayoielewa?

You, Salama,
Come...

You. Salama, very beautiful.
Sitaki mwalimu.

Igizo limeisha.
Basi, basi. Ndiyo maana sitaki mwanangu aende Sekondari.
Shule gani isiyo na elimu ndani yake. Zinawaharibu vijana tu!

Si kweli. Hawa wanajitakia wenyewe. waache utoro. Hawataki kusoma.
Hapana mwalimu. Weka mazingira ya kusoma watasoma tu!
Tutavumilia hadi lini?

Tusikilizane. Ukweli ni kwamba hali haitabadilika kwa siku hizi chache. Tutafute njia mbadala.
Hapana, hii ni kazi ya serikali.

Ni kweli. Lakini sisi pia ni serikali. Tutangoja mpaka lini? Mimi najitolea kufundisha saa tatu kwa wiki. Naomba na wengine wajitolee.
Na sisi wawezeshaji rika tutafundisha stadi za maisha kila jioni, tukiruhusiwa.

Lakini kwa nini hakuna vitabu? Ina maana Serikali haitoi fedha?
Mbona ipo? Hii ruzuku ya kila mwanafunzi inaenda wapi? shilingi 25,000 kila mwanafunzi!
Jamani tuunde kamati ya kumwona Afisa Elimu. Haiwezekani shule ya kata igeuke Shule ya ukata.

Sikutaka kwenda sekondari, nilijua sina Kiingereza cha kutosha. Nang'ang'ania ung'eng'e wa nini?
Ni kweli, bora pawe na masomo ya ziada kwa Kiswahili. Kiingereza si elimu. Uelewa ndio elimu.

Na tuweke kompyuta. Ziko za umeme wajua siku hizi. kisha wanaweza kutafuta habari kwa kompyuta.
Wazazi mkiamka namna hiyo, hata sisi walimu tutapata nguvu zaidi.

Je wajua?

1. Viwango vya shule za sekondari vilivyowekwa na Wizara ya Elimu ni kama vifuatavyo:

    - Mwalimu mmoja kwa kila wanafunzi 30
    - Kila mwanafunzi awe na kitabu kwa kila somo
    - Shule zote za kutwa zitoe chakula cha mchana

    Hivi viwango vimefikiwa kiasi gani huko kwenu?

2. Katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) Serikali iliazimia kupeleka mashuleni shilingi 25,000 kwa kila mwanafunzi. Lakini kwa wastani pesa zilizopelekwa ni shilingi 7,634[1].

3. Walimu walio wengi sana wana stashahada tu wakati sera ya elimu inasema kwamba, kuanzia Kidato cha Tatu, wanafunzi wafundishwe na walimu wenye shahada tu.

4. Mwaka 2009, shule 150 tu zilikuwa na maabara ya sayansi, karibu zote zikiwa shule za zamani.

5. Hata mwaka 1984[2], utafiti ulionyesha kwamba 10% tu ya wanafunzi waliopo Kidato cha Nne walikuwa na Kiingereza cha kutosha kuwawezesha kusoma masomo yote kwa lugha hiyo. Hali sasa ni mbaya zaidi. Utafiti uliofanywa na TAMASHA wakishirikiana na Twaweza, uligundua kwamba chini ya robo ya wanafunzi waliweza kusoma kipande cha Kiingereza cha darasa la pili na kujibu maswali juu yake[3]. Zaidi ya nusu hawakuweza kujibu maswali kabisa.

---

1 HakiElimu na Twaweza (2011)
2 Criper and Dodd
3 Elimu Dhalimu (2011)

Tufanye nini?

Kwa hali ilivyo serikali haina uwezo wa kuhudumia kila shule ipasavyo. Hivyo, wakati tunafuatilia utoaji na matumizi ya ruzuku ya shule, inawezekana pia kupanua uwezo wa wanafunzi kupata elimu kwa:

- Kuwakaribisha walimu na wataalam wengine waliostaafu waliopo kwenye jamii.
- Kununua taa za solar (umeme wa jua) ili wanafunzi waweze kusoma usiku.
- Kuweka kompyuta zinazotumia umeme wa jua. Kwa njia hiyo mtoto anaweza kutafuta taarifa anazotaka mwenyewe.
- Kutengeneza zana nyingi kwa lugha ya Kiswahili. Watoto wakishaelewa dhana vizuri, ni rahisi zaidi kuelewa Kiingereza chake.

Mwisho tujiulize:

- Wangapi tumenunua kitabu cha kiada kwa ajili ya watoto wetu?
- Wangapi tumenunua kitabu cha hadithi au burudani ili kujenga hamu na raha ya kusoma?

Shindano

Toa maoni, jishindie kompyuta!

Ndugu msomaji, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imeahidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia mpango huu, Serikali inataka kukusikia.

Toa maoni yako kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii; maji, elimu na afya.

Tuambie wazo moja kuboresha elimu, afya au maji. Halafu, tuambie mwananchi afanye nini kuleta mabadiliko.

Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2013, maoni kumi bora yatachaguliwa na kila shule itakayotoa washindi itapatiwa kompyuta ndogo mbili (laptops). Pia, maoni ya washindi yatachapishwa kwenye vitabu na tovuti.

Sharti: Kila mtu anaweza kutuma maoni, lakini zawadi zitatolewa kwa watakaondika *kupitia* shule zao tu.

Tuma maoni yako kabla ya tarehe 1 Novemba, 2013

Anuani: OGP Tanzania, S.L.P 38342, Dar es Salaam

Barua pepe: unasemaje@gmail.com

Kumbuka kuweka taarifa hizi:

- Tarehe
- Majina kamili, umri wako, jina la shule; jinsia (me/ke)
- Anuani kamili: SLP na makazi (kata, wilaya na mkoa); namba ya simu; barua pepe

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi **(Open Government Partnership - OGP).**

Open Government Partnership

Mpango wa OGP unahimiza shughuli za Serikali ziendeshwe kwa uwazi zaidi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, mwitikio wa Serikali, kupambana na rushwa na kujenga kuaminika zaidi. Twaweza inashirikiana na Serikali kuendeleza uwazi na ushiriki wa wananchi kupitia Mpango wa OGP.